BENKI KUU YA TANZANIA
1966-2026

BENKI KUU YA TANZANIA



# Tathmini Ya Mwenendo Wa Uchumi

Machi 2026

# Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ........ 1
2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa ........ 3
2.1 Mfumuko wa Bei ........ 3
2.2 Sera ya Fedha ........ 6
2.3 Viwango vya Riba ........ 8
2.4 Masoko ya Fedha ........ 8
2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ........ 9
2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa ........ 10
2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje ........ 12
3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar ........ 15
3.1 Mfumuko wa Bei ........ 15
3.2 Bajeti ya Serikali ........ 15
3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje ........ 16
Viambatisho ........ 18
Tafsiri ya Dhana Muhimu ........ 31

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliendelea kukua kwa kasi ya wastani mwezi Februari 2026, ukichochewa na kuongezeka kwa matumizi binafsi, uwekezaji unaoendelea katika miradi ya kiteknologia na miundombinu, pamoja na kupungua taratibu kwa masharti ya kifedha[1]. Nchi zilizoendelea kiuchumi zilionesha ukuaji chanya ila usio sawa, ukichangiwa na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji viwandani na sekta ya huduma. Hata hivyo, kasi ukuaji wake kwa ujumla bado upo chini ya wastani wa ukuaji wa muda mrefu ikichagizwa na mtazamo wa kibiashara unaoendelea kuwa wa tahadhari[2].

Katika nchi zinazoibukia kiuchumi, shughuli za kiuchumi ziliendelea kunufaika na sera za ndani na uwekezaji, ingawa kulikuwa na tofauti ya ukuaji kati ya kanda na sekta. Aidha, katika ukanda wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, matarajio ya muda mfupi yalionyesha viwango vya uthabiti, ingawa yaliathiriwa na masharti magumu ya fedha kutoka nje na ongezeko la hatari ya kufungwa kwa mlango Bahari wa Hormuz na athari zake katika bishara za kikanda na usambazaji wa nishati.

Mizani ya vihatarishi vya matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kuelemea upande wa kushuka. Mivutano inayoendelea ya sera za biashara pamoja na kuongezeka kwa hali ya kutotabirika kwa siasa duniani vinaendelea kufifisha mwelekeo wa ukuaji wa muda mfupi, jambo linaloonekana katika kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi duniani na kupanda kwa gharama za usafirishaji na bei ya nishati (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b).

[1] Benki ya Dunia, Taarifa ya Kila Mwezi ya Dunia: Februari 2026

[2] Mapitio ya Uchumi ya OECD, Ripoti ya Muda ya Mwezi Machi 2026: Kupima Ustahimilivu

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Kwa mwezi Februari 2026, bei za bidhaa duniani zilionesha mwenendo tofauti, zikiakisi misingi isiyo sawa ya ugavi na mahitaji pamoja na kuongezeka kwa hisia za hatari. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, bei ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 5.6 ikichochewa na kuongezeka kwa uhitaji wa hifadhi salama ya mali kutokana na mvutano unaoendelea Mashariki ya Kati na ununuzi endelevu wa Benki Kuu mbalimbali duniani. Bei ya kahawa na kakao ilishuka kufuatia kushuka kwa wasiwasi wa ugavi, huku bei ya mafuta ya kula ikiimarika, ambapo kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi bei ya mafuta ya mawese iliongezeka kwa asilimia 3.7, ikichangiwa na msimu mdogo wa uzalishaji Kusini Mashariki mwa Asia na kuongezeka kwa mahitaji duniani. Bei za nafaka ziliongezeka, ambapo bei ya ngano iliongezeka kwa asilimia 3.1 kutokana na wasiwasi wa kupungua kwa

uzalishaji kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa Ulaya na Marekani. Kwa upande mwingine, bei ya sukari ilishuka kwa asilimia 4.1 kufuatia matarajio chanya ya upatikanaji wa bidhaa hiyo. Bei za mbolea zilipanda kwa asilimia 6.5 kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, huku bei ya urea ikiongezeka kwa kasi ya asilimia 13.6, ikionyesha athari za uzalishaji zinazohusiana na kupanda kwa gharama za nishati pamoja na gharama za uzalishaji (Kielelezo 1.2 na Jedwali A8).

**Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




Chanzo: Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects
Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

Ingawa bei za bidhaa duniani zimeendelea kupanda, kwa ujumla mfumuko wa bei duniani kwa mwezi Februari 2026 uliendelea kuwa wa wastani, ukitofautiana kati ya nchi na nchi. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei uliendelea kudhibitiwa. Nchini Marekani, mfumuko wa bei uliendelea kuwa thabiti, huku gharama za mishahara zikipunguza athari za kupanda kwa gharama za nishati. Katika eneo la Ulaya, mfumuko wa bei uliongezeka kwa kiasi kidogo kufuatia kupanda kwa bei za huduma mbalimbali, huku nchini Uingereza, mfumuko wa bei ukipungua kwa kiwango kidogo kutokana na athari za kubana sera za kifedha na hatua zilizochukuliwa awali zinazoendelea kuathiri uchumi mpana.

Kwa upande wa nchi zinazoibukia kiuchumi, mwenendo wa mfumuko wa bei ulikuwa mchanganyiko, ukichangiwa kwa kiasi kikubwa tofauti za mazingira ya kiuchumi kati ya nchi na nchi. China ilionyesha ongezeko la muda mfupi lililotokana zaidi na kupanda kwa bei ya vyakula wakati wa sikukuu ya mwaka mpya wa nchi hiyo. Mfumuko wa bei nchini India uliongezeka kidogo kutokana na mahitaji makubwa ya ndani na uboreshaji wa miundombinu, ingawa uliendelea kubaki ndani ya wigo unaokubalika. Katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei kwa ujumla uliendelea kuwa wa kuridhisha. Kikanda (Jumuiya ya Afrika Mashariki, EAC, na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, SADC), nchi nyingi zilibaki ndani ya viwango vya ulinganifu wa mtangamano, ukichangiwa na kuimarika kwa mavuno na uthabiti wa sera ya fedha (Jedwali 1.1, Kielelezo 1.3 Kielelezo 1.4, na Kielelezo 1.5).

**Jedwali 1.1: Mienendo na Vichocheo vya Mfumuko wa Bei Duniani**

| Kanda/Nchi | Feb-26 (%, mwaka kwa mwaka) | Mabadiliko Kati ya Feb-26 na Jan-26 | Vichocheo vikuu |
|---|---|---|---|
| Marekani | 2.4 | Imara | Kupoa kwa soko la ajira (msingi 2.5% dhidi ya nishati +0.5%). |
| Ukanda wa Euro | 1.9 | Kuongezeka kidogo | Mfumuko wa bei wa huduma 3.4% (dhidi ya 3.2% Januari 2026). ulisababisha ongezeko |
| China | 1.3 | Ongezeko la muda mfupi | Athari za Mwaka Mpya wa Lunar ziliongeza bei za chakula na huduma |
| EAC ï wastani wa kikanda | 5.9 | Kupungua | Kupungua kwa jumla katika usafiri, huduma za umma na shinikizo za huduma |
| SADC ï wastani wa kikanda | 5.9 | Kupungua | Kupungua kwa bei za mafuta na usafiri pamoja na kupungua kwa bei za chakula |

Chanzo: IMF/OECD na Ofisi za Takwimu za Taifa

Tanbihi: [1]Wastani usio na uzito, uliokokotolewa kutoka Kenya asilimia 4.3, Tanzania asilimia 3.2, Uganda asilimia 2.9, Rwanda asilimia 7.9, Burundi asilimia 11.4 (zote Feb-26). Hii imepungua kutoka asilimia 6.2 mwezi Jan 2026.

[2]Wastani usio na uzito, uliokokotolewa kutoka nchi 12 zenye data za Feb-26 (Angola 13.4, Botswana 4.0, Lesotho 2.7, Malawi 24.1, Mauritius 3.5, Msumbiji 3.2, Namibia 2.4, Shelisheli 0.3, Afrika Kusini 3.0, Tanzania 3.2, Zambia 7.5, na Zimbabwe 3.8 – zote kwa asilimia). Hii imepungua kutoka wastani wa kundi hilo hilo wa Jan-26 (asilimia 6.7).

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei Kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**



Chanzo: Ofisi za Taifa za Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Kwa mwezi Februari 2026, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2, sawa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Utulivu huo unaakisi athari halisi ya kupungua kwa mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi na nishati, hali ambayo kwa kiasi kikubwa imeweza kufidia ongezeko la kimsimu katika bei ya vyakula. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mfumuko wa bei ulipungua kidogo kutoka asilimia 3.3 mwezi Januari 2026, ikiwa ndani ya malengo ya kitaifa na sambamba na vigezo vya mtangamano wa SADC and EAC (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1).

## Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

| | | Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Feb-25 | Jan-26 | Feb-26 | Feb-25 | Jan-26 | Feb-26 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 1.2 | 0.3 | 1.2 | 5.0 | 5.7 | 5.7 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 0.1 | 0.2 | 0.0 | 3.5 | 2.2 | 2.1 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | 0.2 | 0.0 | 0.0 | 2.0 | 1.2 | 1.1 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | 0.9 | 0.2 | 0.4 | 3.1 | 2.3 | 1.7 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 2.2 | 2.7 | 2.5 |
| Afya | 2.5 | 0.2 | 0.1 | 0.0 | 1.2 | 1.1 | 0.9 |
| Usafiri | 14.1 | 0.3 | 0.2 | 0.1 | 3.2 | 4.2 | 4.0 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | 0.0 | 0.2 | 0.2 | 0.0 | 0.9 | 1.1 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 0.1 | 0.6 | 0.1 | 1.7 | 0.6 | 0.6 |
| Elimu | 2.0 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 4.2 | 0.4 | 0.3 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.0 | 0.3 | 0.6 | 1.8 | 1.1 | 1.7 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.7 | 0.5 | 0.3 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.1 | 2.9 | 0.0 | 3.3 | 3.2 | 3.2 |
| Fahirisi Bidhaa Zote | 100.0 | 0.6 | 0.2 | 0.5 | 3.2 | 3.3 | 3.2 |
| Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Faharisi ya Bidhaa za Msingi | 73.9 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 2.5 | 2.2 | 2.1 |
| Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi | 26.1 | 1.6 | 0.4 | 1.4 | 5.0 | 6.0 | 5.9 |
| Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | 2.3 | -0.1 | 0.5 | 5.4 | 5.2 | 2.8 |
| Fahirisi za Huduma | 37.2 | 0.1 | 0.3 | 0.2 | 1.4 | 4.6 | 2.2 |
| Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 0.9 | 0.2 | 0.6 | 4.2 | 2.1 | 3.7 |
| Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 4.0 | 3.9 | 0.3 |
| Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji  Visivyo na Kilevi | 71.8 | 0.3 | 0.2 | 0.2 | 2.4 | 2.2 | 2.1 |

Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei ya bidhaa za msingi ulikuwa na mchango mkubwa katika mfumuko wa bei wa jumla kwa mwezi Februari 2026, ukichangia asilimia 1.6, pungufu kidogo kutoka asilimia 1.7 ya mwezi uliopita. Mchango wa vyakula visivyochochakatwa uliongezeka kidogo kufikia asilimia 1.4 kutoka asilimia 1.3  mwezi Januari 2026, ukiakisi mabadiliko ya kimsimu. Vilevile, katika mwezi wa mapitio, mchango wa fahirisi ya nishati uliendelea kuwa imara kwa asilimia 0.2, sambamba na kupungua kwa bei ya nishati (Kielelezo 2.1.2).

## Kielelezo 2.1.2: Mchango Katika Mfumuko wa Bei

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi usiohusisha vyakula na nishati vyenye mabadiliko makubwa ya bei ulipungua hadi asilimia 2.1 mwezi Februari 2026, kutoka asilimia 2.2 mwezi kama huo mwaka 2025. Kwa kiasi kikubwa, punguzo hilo lilitokana na kasi ndogo ya ongezeko la bei ya bidhaa zisizo za kudumu na za kudumu kwa muda wa kati, hasa mavazi, viatu, samani, na vifaa vya nyumbani, pamoja na gharama zinazohusiana na matengenezo ya kawaida ya nyumbani (Kielelezo 2.1.3 na Jedwali 2.1.1).

## Kielelezo 2.1.3: Viwango vya Mfumuko wa bei kwa Miezi Kumi na Mbili

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa vyakula ulikuwa asilimia 5.7, sawa na mwezi uliotangulia, ingawa uliendelea kuwa juu ukilinganishwa na asilimia 5 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Hali hii inaakisi uwiano wa kimsimu katika usambazaji na upatikanaji wa mazao, sambamba na kupungua kwa bei za vyakula  vikuu na

vyakula mbadala, hususan maharage na uwele (Kielelezo 2.1.4a na Kielelezo 2.1.4b).

**Kielelezo 2.1.4: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao**

a. **Mazao ya Vyakula Vikuu**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

b. **Mazao ya Vyakula Mbadala**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula inayohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula nchini ilikuwa tani 560,007.9 mwezi Februari 2026 ikilinganishwa na tani 567,469.2 mwezi uliopita, kutokana na mauzo ya tani 7,461.3 za mahindi na mpunga kwa wafanyabiashara nchini (Jedwali 2.1.2). Kuuzwa kwa kiasi hiki sokoni kulisaidia kudumisha utulivu wa bei ya rejareja ya vyakula sokoni.

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 | 567,469 |
| Feb | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 | 560,008 |
| Mac | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 | |
| Apr | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 | |
| Mei | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 | |
| Jun | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 | |
| Jul | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 | |
| Ago | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 | |
| Sep | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 | |
| Okt | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 | |
| Nov | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 | |
| Des | 137,655 | 248,282 | 677,115 | 577,376 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

Mfumuko wa bei ya nishati, mafuta na huduma za msingi ulishuka hadi asilimia 2.8 Februari 2026, kutoka asilimia 5.2 mwezi uliopita na ulikuwa chini ya asilimia 5.4 iliyorekodiwa mwezi kama huo 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.4). Kwa kiasi kikubwa mwenendo wa kupungua ulitokana na utulivu wa bei ya mkaa na kuni. Bei ya rejareja ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ilikuwa na mwelekeo wa kupungua katika kipindi hicho, ikiakisi kupungua kwa bei za mafuta duniani (Kielelezo 2.1.5).

**Kielelezo 2.1.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

TZS kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

## 2.2 Sera ya Fedha

Kama ilivyonukuliwa katika mapitio yaliyopita, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC), katika kikao kilichofanyika Januari 2026, ilibakiza riba ya Benki Kuu (CBR) kuwa asilimia 5.75 kwa robo inayoishia Machi 2026. Hivyo, utekelezaji wa sera katika mwezi Februari 2026, ulilenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki "*7-day IBCM rate*" inabaki ndani ya wigo wa asilimia 2 juu na chini ya CBR *(+/- 2 percent of CRB rate)*. Hivyo, riba ya mikopo ya siku 7 ilibaki karibu na CBR huku kikidumisha ukwasi wa kutosha wa shilingi katika mfumo wa kibenki ( Kielelezo 2.2.1 na Kielelezo 2.2.2).

**Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana uliendelea kuongezeka sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3), ulikua kwa asilimia 24.5 ikiendeleza kasi iliyorekiwa mwezi Januari 2026 (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la ukuaji wa mkopo kwa sekta binafsi. Mikopo kwa sekta binafsi iliSSyoongezeka kufikia asilimia 24.4 kutoka asilimia 23.5 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.4, Kielelezo 2.2.5 na Jedwali 2.2.1).

**Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake**

| | Kiasi (Shilingi Billioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipengele | Feb-25 | Jan-26 | Feb-26 | Feb-25 | Jan-26 | Feb-26 |
| Rasilimali halisi za nje | 14,706.2 | 15,950.0 | 15,652.8 | 43.6 | 25.7 | 6.4 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 13,020.1 | 13,987.7 | 13,992.5 | 18.1 | 28.0 | 7.5 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,686.1 | 1,962.3 | 1,660.3 | --- | 11.4 | -1.5 |
| Rasilimali halisi za ndani | 35,942.2 | 46,155.7 | 47,416.5 | 6.6 | 24.3 | 31.9 |
| Madai rasmi ya ndani | 48,836.1 | 57,872.1 | 58,849.3 | 8.5 | 17.5 | 20.5 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na | 7,987.3 | 9,705.7 | 9,956.8 | -8.0 | 20.6 | 24.7 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 36,982.7 | 45,171.4 | 46,007.4 | 13.2 | 23.5 | 24.4 |
| Rasilimali nyinginezo | -12,893.9 | -11,716.5 | -11,432.8 | 14.4 | -3.2 | -11.3 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 50,648.4 | 62,105.7 | 63,069.3 | 15.2 | 24.6 | 24.5 |
| Amana za fedha za kigeni | 12,818.2 | 14,103.2 | 14,569.7 | 26.5 | 13.6 | 13.7 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 37,830.2 | 48,002.5 | 48,499.6 | 11.8 | 28.3 | 28.2 |
| Amana zinginezo | 14,711.5 | 18,229.5 | 18,541.9 | 10.7 | 27.1 | 26.0 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 23,118.8 | 29,773.0 | 29,957.7 | 12.5 | 29.0 | 29.6 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 6,954.5 | 8,102.1 | 8,151.8 | 14.3 | 15.8 | 17.2 |
| Amana za hundi | 16,164.2 | 21,670.9 | 21,805.9 | 11.8 | 34.8 | 34.9 |
| Fedha za msingi (M0) | 12,078.7 | 15,225.1 | 14,990.0 | 19.1 | 30.5 | 24.1 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Mikopo kwa shughuli za madini na uchimbaji mawe ilirekodi ongezeko la juu zaidi, ikipanda kwa asilimia 103.9, ambalo ni ongezeko la juu zaidi tangu mwanzoni mwa mwaka 2025. Ukuaji huu uliendelea kuchangiwa na jitihada za kimkakati za Serikali zinazolenga kuboresha sekta ya uanzishwaji wa uboreshaji wa huduma za fedha jumuishi kwa wachimbaji wadogo kwa kutumia dhamana mbalimbali.

Wachangiaji wengine katika ukuaji wa mikopo walijumuisha shughuli za biashara, ambazo zilipanuka kwa asilimia 48.7, zikibadilisha mwenendo wa wastani wa mwaka uliopita, ikifuatiwa na usafirishaji na mawasiliano, ambavyo vilikuwa kwa asilimia 39.4 (Jedwali 2.2.2). Kuongezeka kwa mikopo ya biashara kunadhihirisha ongezeko la shughuli za kibiashara nchini, huku kukua kwa mikopo ya kilimo (asilimia 31.9), kwa sehemu kubwa kulichangiwa na uwepo wa mikopo maalum kupitia dirisha la mikopo kwa sekta hiyo kwa mabenki kutoka Benki Kuu iliyolenga kuongeza tija katika sekta ya kilimo. Kwa upande mwingine, mikopo katika shughuli za uzalishaji viwandani iliendelea kupungua hadi kufikia ukuaji wa hasi kwa asilimia 8.5 mwezi Februari 2026. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na urejeshwaji wa mikopo iliyokuwepo.

### Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi

Asilimia

| | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 | Des-25 | Jan-26 | Feb-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini | -28.2 | -24.8 | -10.5 | 91.1 | 91.4 | 103.9 |
| Biashara | 5.8 | 12.7 | 14.4 | 49.7 | 50.0 | 48.7 |
| Kilimo | 14.5 | 22.4 | 29.8 | 29.4 | 34.2 | 39.4 |
| Ujenzi | 37.2 | 36.3 | 39.2 | 28.9 | 27.9 | 31.9 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 23.1 | 35.1 | 23.8 | 25.6 | 29.5 | 28.1 |
| Hoteli na migahawa | 13.1 | 9.4 | 7.0 | 17.7 | 17.8 | 18.9 |
| Shughuli binafsi | 4.6 | 5.4 | 14.7 | 2.5 | 1.6 | 5.2 |
| Viwanda | 16.9 | 10.9 | 7.7 | -8.2 | -7.7 | -8.5 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Mikopo kwa shughuli binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa hutumika kugharamia shughuli za wajasiriliamali wadogo sana, wadogo, na wakati, iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote ya sekta binafsi kwa asilimia 35.4, ikifuatiwa na biashara (asilimia 14.7) na kilimo (asilimia 13.7) (Kielelezo 2.2.6).

### Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.3 Viwango vya Riba

Katika mwezi Februari 2026, viwango vya riba vya mabenki vilikuwa tulivu. Riba za mikopo kwa ujumla hazikuwa na mabadiliko makubwa, zikifikia asilimia 15.11 kutoka asilimia 15.10 mwezi Januari 2026. Riba za mikopo ya wateja wakubwa (negotiated lending rates) zilipungua hadi asilimia 12.19, ikilinganishwa na asilimia 12.25 mwezi uliopita. Kwa upande wa amana, riba kwa ujumla ilikuwa asilimia 8.32, ikipungua kutoka asilimia 8.33 mwezi Januari 2026, huku riba za amana kwa wateja wakubwa zilipungua hadi asilimia 11.48 kutoka asilimia 11.74. Kufuatia mwenendo huu, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.59, kutoka asilimia 5.79 mwezi Januari 2026 (Jedwali 2.3.1).

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa na Benki za Biashara**

Asilimia

| | Feb-25 | Mac-25 | Des-25 | Jan-26 | Feb-26 |
|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.98 | 2.86 | 3.02 | 2.94 | 2.98 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.14 | 15.50 | 15.24 | 15.10 | 15.11 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.77 | 15.83 | 15.46 | 15.49 | 15.41 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 13.42 | 12.94 | 12.38 | 12.25 | 12.19 |
| Riba za amana -jumla | 8.13 | 8.00 | 8.36 | 8.33 | 8.32 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.48 | 8.14 | 9.58 | 9.70 | 9.82 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 11.40 | 10.35 | 11.66 | 11.74 | 11.48 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 6.29 | 7.69 | 5.88 | 5.79 | 5.59 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Masoko ya Fedha

### Soko la dhamana za Serikali

Dhamana za Serikali ziliendelea kuwa na mahitaji makubwa kuliko ilivyotarajiwa, huku hali ya utulivu wa uchumi ikiendelea kuvutia wawekezaji hususani katika hati fungani. Benki Kuu ilifanya minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi zenye thamani ya shilingi bilioni 440.9, ambazo zilitumika kugharamia matumizi ya Serikali na utekelezaji wa sera ya fedha. Minada ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 1,061.4, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 431.1 zilikubaliwa (Kielelezo 2.4.1). Kufuatia mwenendo huu, wastani wa riba ya jumla ya dhamana za Serikali ulipungua hadi kufikia asilimia 5.68 kutoka asilimia 5.89 mwezi uliotangulia. Mwelekeo huu wa kupungua kwa riba unaashiria imani ya soko na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika mfumo wa benki.

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Benki Kuu ilifanya minada ya hati fungani za serikali za miaka 15 na 25, zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 399.5 kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali. Minada hii ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 2,778.1, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 520.2 zilikubaliwa. Wastani wa riba (weighted average yields) za hati fungani za miaka 15 na 25 zilipungua hadi asilimia 10.78 na asilimia 11.99, mtawalia.

### Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki (IBCM) liliendelea kuwezesha ukwasi wa shilingi baina ya mabenki. Katika mwezi Februari 2026, mauzo katika soko yalipungua hadi shilingi bilioni 2,796.5 kutoka shilingi bilioni 2,868.9 mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.2). Soko lilitawaliwa na mikopo ya siku saba, ambayo ni asilimia 63.5 ya mikopo yote, ikionesha mabenki kupendelea mikopo ya siku saba badala ya ile ya siku moja (overnight).

Ikiakisi uwepo wa ukwasi wa kutosha katika mfumo wa kibenki, riba ya jumla ilipungua hadi wastani wa asilimia 6.34 kutoka asilimia 6.40 iliyorekodiwa mwezi Januari 2026. Kupungua kwa kiwango cha riba cha soko la fedha kati ya

mabenki, na utulivu wa viwango vya riba ya siku moja (overnight) na siku saba (7), kunaonesha ufanisi wa mwelekeo wa sasa wa sera ya fedha katika kudhibiti viwango vya riba vya soko kuwa karibu na CBR.

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Soko la fedha za kigeni

Hali ya ukwasi wa fedha za kigeni katika uchumi uliendelea kuimarika katika kipindi cha mapitio, ikichangiwa na ongezeko la mauzo ya nje ya mazao ya asili na madini. Kufuatia mwenendo huu, mauzo ya fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni (IFEM) yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 184.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 88.2 zilizouzwa mwezi uliotangulia. Benki Kuu ilishiriki katika soko kwa kuuza jumla ya Dola milioni 128.8, ikilinganishwa na Dola milioni 58 mwezi uliopita (Kielelezo 2.4.3).

Thamani ya shilingi ya Tanzania ilikuwa na wastani wa TZS 2,570.24 kwa Dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na TZS 2,492.05 kwa Dola moja ya Marekani mwezi kama huo mwaka 2025. Hii ni sawa na kushuka kwa thamani ya shilingi kwa asilimia 3.14 kwa mwaka.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwezi Januari 2026 yaliendelea kuwa mazuri, yakifikia kiasi cha shilingi bilioni 3,340.2, yakizidi malengo kwa asilimia 5.4. Mapato ya Serikali Kuu yalikuwa shilingi bilioni 3,156.4 na kiasi kilichobaki yalikuwa makusanyo kutoka Serikali za Mitaa.

Mapato ya kodi yaliendelea kuwa ya kuridhisha, yakifikia shilingi bilioni 2,762.3, zaidi ya lengo la mwezi kwa asilimia 7.1. Matokeo hayo yaliendelea kuonesha mchango chanya wa usimamizi wa kodi na kuimarika kwa uzingatiaji wa ulipaji kodi. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 394.1, sawa na asilimia 87.9 ya lengo (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi January**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Serikali iliendelea kuwianisha matumizi yake na mapato. Jumla ya matumizi ya Serikali katika mwezi Januari 2026 yalifikia shilingi bilioni 3,751.7, ambapo shilingi bilioni 2,689.9 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 1,061.8 zikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Januari**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Hadi mwishoni mwa mwezi Februari 2026, deni la Taifa lilikuwa dola za Marekani milioni 51,112.8, likipungua kwa asilimia 0.2 ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwishoni wa mwezi Januari 2026. Kati ya kiasi hiki, deni la nje lilikuwa asilimia 70.2 (Kiambatisho, Jedwali A10).

### Deni la Nje

Deni la nje (la umma na binafsi) lilipungua kwa asilimia 0.1 hadi dola za Marekani milioni 35,859.1 mwishoni mwa mwezi Februari 2026. Kati ya kiasi hicho, asilimia 82.7 ilikuwa deni la nje la Serikali, na sehemu iliyobaki ilikuwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1).

Mikopo ya nje iliyopokelewa katika mwezi Februari 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 83.8, sehemu kubwa ikipokelewa na Serikali Kuu. Kiasi cha dola za Marekani milioni 98.9 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 35.4 zilitumika kufanya malipo ya mkopo mkuu.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji ulikuwa sawa na mwezi uliopita, ambapo mashirika ya fedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu kwa asilimia 57.8, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Mikopo ya urari wa malipo ya nje, na utekelezaji wa bajeti (BoP and budget support) iliongoza kwa matumizi ya mikopo yote iliyopokelewa, ikifuatiwa na mikopo kwenda kwenye shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani ikiendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 66, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya, Euro (Jedwali 2.6.3 na Jedwali 2.6.4).

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| | Feb-25 | | Jan-26$^{r}$ | | Feb-26$^{p}$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Serikali Kuu | 26,394.4 | 80.5 | 29,687.2 | 82.7 | 29,640.4 | 82.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 26,317.1 | 80.3 | 29,606.9 | 82.5 | 29,560.2 | 82.4 |
| Malimbikizo ya riba | 77.3 | 0.2 | 80.3 | 0.2 | 80.2 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 6,389.9 | 19.5 | 6,204.7 | 17.3 | 6,218.7 | 17.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,827.2 | 17.8 | 5,770.3 | 16.1 | 5,774.3 | 16.1 |
| Malimbikizo ya riba | 562.8 | 1.7 | 434.3 | 1.2 | 444.5 | 1.2 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 32,788.0 | 100.0 | 35,891.9 | 100.0 | 35,859.1 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| | Feb-25 | | Jan-26$^{r}$ | | Feb-26$^{p}$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,366.1 | 56.0 | 20,788.2 | 57.9 | 20,730.5 | 57.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,335.1 | 55.9 | 20,765.1 | 57.9 | 20,707.6 | 57.7 |
| Malimbikizo ya riba | 31.0 | 0.1 | 23.2 | 0.1 | 22.9 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,349.5 | 4.1 | 1,591.6 | 4.4 | 1,581.3 | 4.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,272.2 | 3.9 | 1,511.3 | 4.2 | 1,501.1 | 4.2 |
| Malimbikizo ya riba | 77.3 | 0.2 | 80.3 | 0.2 | 80.2 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,918.0 | 36.3 | 12,786.3 | 35.6 | 12,818.5 | 35.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 11,557.7 | 35.2 | 12,427.9 | 34.6 | 12,452.9 | 34.7 |
| Malimbikizo ya riba | 360.3 | 1.1 | 358.4 | 1.0 | 365.6 | 1.0 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,154.5 | 3.5 | 725.7 | 2.0 | 728.8 | 2.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 983.0 | 3.0 | 672.9 | 1.9 | 672.9 | 1.9 |
| Malimbikizo ya riba | 171.5 | 0.5 | 52.8 | 0.1 | 55.9 | 0.2 |
| Jumla ya deni la nje | 32,788.0 | 100.0 | 35,891.9 | 100.0 | 35,859.1 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

### Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa Asilimia

| Shughuli ya uchumi | Feb-25 Amount | Feb-25 Share (%) | Jan-26[r] Amount | Jan-26[r] Share (%) | Feb-26[p] Amount | Feb-26[p] Share (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 6,713.2 | 20.9 | 7,982.8 | 22.6 | 7,959.6 | 22.5 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 6,813.0 | 21.2 | 7,711.8 | 21.8 | 7,738.7 | 21.9 |
| Kilimo | 1,552.5 | 4.8 | 1,871.1 | 5.3 | 1,878.0 | 5.3 |
| Nishati na madini | 4,213.9 | 13.1 | 4,248.3 | 12.0 | 4,242.2 | 12.0 |
| Viwanda | 1,145.1 | 3.6 | 1,320.2 | 3.7 | 1,321.0 | 3.7 |
| Huduma za jamii na elimu | 6,424.6 | 20.0 | 6,869.4 | 19.4 | 6,830.1 | 19.3 |
| Fedha na bima | 1,459.0 | 4.5 | 1,255.4 | 3.5 | 1,253.4 | 3.5 |
| Utalii | 511.9 | 1.6 | 635.9 | 1.8 | 634.5 | 1.8 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 1,545.6 | 4.8 | 1,743.0 | 4.9 | 1,742.6 | 4.9 |
| Mengineyo | 1,769.3 | 5.5 | 1,739.3 | 4.9 | 1,734.3 | 4.9 |
| Jumla | 32,148.0 | 100.0 | 35,377.2 | 100.0 | 35,334.4 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali.

### Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia

| Sarafu | Feb-25 | Jan-26[r] | Feb-26[p] |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 67.6 | 65.9 | 66.0 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 16.7 | 17.7 | 17.7 |
| Yuan ya China | 6.3 | 6.5 | 6.5 |
| Sarafu nyinginezo | 9.3 | 9.8 | 9.8 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Mwisho wa Februari 2026, deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 38,781.7, sawa na ongezeko la asilimia 0.5 (Kielelezo 2.6.1). Sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali ilibaki kuwa hati fungani, huku benki za biashara na mifuko ya hifadhi za jamii zikiendelea kuwa wadai wakuu kwa asilimia 54.9 ya deni lote (Jedwali 2.6.5 na Jedwali 2.6.6).

### Kielelezo 2.6.1: Deni la Ndani la Serikali Kuu

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha

### Jedwali 2.6.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo

Shilingi Bilioni

| Nyenzo | Feb-25 Kiasi | Feb-25 Mchango (%) | Jan-26 Kiasi | Jan-26 Mchango (%) | Feb-26[P] Kiasi | Feb-26[P] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dhamana za serikali | 29,108.2 | 85.6 | 32,972.3 | 85.4 | 33,122.0 | 85.4 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 1,847.4 | 5.4 | 1,821.4 | 4.7 | 1,653.0 | 4.3 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 27,073.7 | 79.6 | 31,015.1 | 80.4 | 31,333.2 | 80.8 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 4,905.9 | 14.4 | 5,627.3 | 14.6 | 5,659.7 | 14.6 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 4,887.5 | 14.4 | 5,627.2 | 14.6 | 5,659.6 | 14.6 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 34,014.1 | 100.0 | 38,599.6 | 100.0 | 38,781.7 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengineyanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

### Jedwali 2.6.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji

Shilingi Bilioni

| Mkopeshaji | Feb-25 Kiasi | Feb-25 Mchango (%) | Jan-26 Kiasi | Jan-26 Mchango (%) | Feb-26[P] Kiasi | Feb-26[P] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za biashara | 9,791.4 | 28.8 | 10,902.5 | 28.2 | 10,834.3 | 27.9 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 6,847.5 | 20.1 | 7,436.0 | 19.3 | 7,468.4 | 19.3 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,097.2 | 26.7 | 10,389.5 | 26.9 | 10,463.9 | 27.0 |
| Kampuni za bima | 1,852.3 | 5.4 | 2,005.0 | 5.2 | 1,983.5 | 5.1 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 552.7 | 1.6 | 737.8 | 1.9 | 757.8 | 2.0 |
| Wengine | 5,872.8 | 17.3 | 7,128.9 | 18.5 | 7,273.8 | 18.8 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 34,014.1 | 100.0 | 38,599.6 | 100.0 | 38,781.7 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na na wawekezaji wasio wakazi

Katika mwezi Februari 2026, Serikali ilikopa kutoka soko la ndani kupitia utoaji wa dhamana za Serikali jumla ya shilingi bilioni 621.9 ambapo shilingi bilioni 450.5 ni hati fungani na shilingi bilioni 171.4 ni dhamana za Serikali za muda mfupi (Kielelezo 2.6.2). Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 875.2 kulipia deni la ndani, ambapo shilingi bilioni 472.2 zilitumika kulipa deni la msingi na shilingi bilioni 403 ni malipo ya riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Mfadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje imeendelea kuwa imara, ikionyesha kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo na kufikia dola za Marekani milioni 2,108.2, kwa mwezi Februari 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,156.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.7.1). Kuimarika huku kulichangiwa na ongezeko la mauzo ya nje ya bidhaa na huduma, hususan mapato yatokanayo na huduma za utalii na dhahabu.

Mwezi Februari 2026, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufika dola za Marekani milioni 6,243.6. Kiasi hiki kinatosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.8 (Kielelezo 2.7.1). Kiwango hiki kipo juu ya lengo la kitaifa la miezi 4 na la vigezo vya mtangamano vya EAC la miezi 4.5 lakini chini kidogo ya kigezo cha miezi 6 cha mtangamano wa SADC.

**Jedwali 2.7.1: Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali**

Dola za Marekani Milioni

| | | | | Mwaka ulioishia Februari | | | Mabadiliko ya asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Feb-25 | Jan-26 | Feb-26[p] | 2024 | 2025 | 2026[p] | |
| Urari wa bidhaa | -228.5 | -292.4 | -287.1 | -5,996.1 | -4,782.3 | -4,406.5 | -7.9 |
| Zilozouzwa nje* | 710.0 | 1,083.6 | 965.2 | 7,794.3 | 9,451.6 | 10,872.9 | 15.0 |
| Zilizonunuliwa nje | 938.5 | 1,376.0 | 1,252.3 | 13,790.4 | 14,233.9 | 15,279.3 | 7.3 |
| Urari wa huduma | 370.35 | 305.3 | 323.6 | 4,010.2 | 4,066.3 | 4,165.5 | 2.4 |
| Mapato | 598.8 | 606.8 | 608.6 | 6,340.1 | 6,913.9 | 7,520.3 | 8.8 |
| Malipo | 228.4 | 301.5 | 285.0 | 2,329.9 | 2,847.6 | 3,354.9 | 17.8 |
| Urari wa bidhaa na huduma | 141.9 | 12.9 | 36.5 | -1,985.9 | -716.0 | -241.0 | -66.3 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,308.8 | 1,690.4 | 1,573.8 | 14,134.4 | 16,365.5 | 18,393.2 | 12.4 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,167.0 | 1,677.5 | 1,537.3 | 16,120.3 | 17,081.5 | 18,634.2 | 9.1 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -162.9 | -199.7 | -218.7 | -1,531.6 | -1,971.8 | -2,133.0 | 8.2 |
| Yaliyoingia | 15.3 | 19.9 | 20.0 | 329.0 | 313.8 | 290.2 | -7.5 |
| Yaliyotoka | 178.2 | 219.7 | 238.7 | 1,860.6 | 2,285.6 | 2,423.2 | 6.0 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 16.9 | 27.7 | 27.7 | 699.6 | 531.5 | 265.8 | -50.0 |
| Iliyoingia | 70.0 | 86.9 | 86.9 | 1,333.1 | 1,120.3 | 906.5 | -19.1 |
| ambapo Serikali | 0.0 | 12.9 | 12.9 | 141.8 | 127.3 | 32.9 | -74.1 |
| Iliyotoka | 53.2 | 59.2 | 59.2 | 633.5 | 588.8 | 640.7 | 8.8 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -4.2 | -159.1 | -154.4 | -2,818.0 | -2,156.3 | -2,108.2 | -2.2 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali
*Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Mauzo ya nje

Mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 12.4 hadi dola za Marekani milioni 18,393.2 katika mwaka ulioisha Februari 2026, kutoka dola za Marekani milioni 16,365.5 katika kipindi kama hicho cha 2025. Ongezeko hili lilitokana zaidi na kuongezeka kwa mapato ya huduma za utalii, ikiashiria urari mzuri wa huduma pamoja na mauzo ya bidhaa hasa dhahabu.

Mauzo ya bidhaa yaliongezeka kwa asilimia 15 hadi dola za Marekani milioni 10,872.9 katika mwaka ulioisha Februari 2026, kutoka dola za Marekani milioni 9,451.6 kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi

na mauzo ya dhahabu, ikichangia asilimia 45.7 ya mauzo yote ya bidhaa, sambamba na bidhaa zilizochakatwa na tumbaku (Kielelezo 2.7.2). Mauzo ya dhahabu yaliongezeka kwa asilimia 35.8 kufikia dola za Marekani milioni 4,968.4 kutoka dola za Marekani milioni 3,658.9, ikichangiwa na kuimarika kwa bei katika soko la dunia. Vilevile, mauzo ya bidhaa za viwandani yalirekodi ukuaji mzuri wa asilimia 26.1 hadi dola za Marekani milioni 1,705.1 kutoka dola za Marekani milioni 1,351.8. Hali hii inaashiria mabadiliko chanya katika uongezaji thamani na kupunguza utegemezi wa mauzo ya malighafi.

Mauzo ya nje ya bidhaa asilia yaliongezeka kwa asilimia 14.5 kufikia dola za Marekani milioni 1,699.6 mwaka ulioisha Februari 2026, ikichangiwa zaidi na mauzo ya tumbaku na kahawa na pamba, na kuimarika kwa bei katika soko la dunia. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya bidhaa yalifikia dola za Marekani milioni 965.2 mwezi Februari 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 710 mwezi kama huo 2025.

**Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Katika kipindi cha mwaka ulioishia Februari 2026, mapato ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 8.8 na kufikia dola za Marekani milioni 7,520.3, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,913.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mapato ya utalii kwa asilimia 4.2, kufikia 2,255,006 (Kielelezo 2.7.3). Vilevile, mapato ya usafirishaji, hususan usafirishaji wa mizigo, yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 2,726 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,385.4 kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mapato ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 608.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 598.8 mwezi Februari 2025.

**Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali
Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

## Uagizaji wa bidhaa na huduma

